Udhamini wa kifedha

Bima ya maisha inaweza kutumiwa kama dhamana kwa mkopo kutoka kwa benki au kwa kampuni ya bima yenyewe. Pesa zinazokopwa huwa ni kima sawa na pesa za kusalimisha bimdhuru kukomaa kwa bima hiyo.

Faida kwa uwekezaji

Bima ya maisha husaidia wanunuzi kufikia malengo makuu maishani. Malengo haya ni pamoja na kununua au kujenga nyumba, kuelimisha watoto katika vyuo vya kati na vyuo vikuu na vilevile kujikimu kimaisha. Bima ya maisha inaweza kutumiwa kuweka pesa ili kuanzisha biashara siku zijazo.

Msamaha wa kodi

Serikali ya Kenya inakubali afueni ya kodi ya asilimia 15 kwa kila malipo ya bima (premium) hadi kiwango cha juu cha shilingi 5,000/=. Afueni hii hutolewa kwenye bima za maisha pekee. Hii ni njia moja ya Serikali ya Kenya kuwavutia watu wengi zaidi kununua bima ya maisha.

“Bima ni mbinu mnununuzi hutumia ili kuhamishia kampuni ya bima mzigo wa hasara za kifedha. Ili apate kusimamiwa na kufidiwa na kampuni ya bima, mnunuzi sharti agharamie malipo ya bima ijulikanayo kwa Kiingereza kama premium.

Insurance Regulatory Authority
Bima Bora kwa Taifa
IRA

IRAKenyaPage @ira_kenya

www.ira.go.ke

Insurance Regulatory Authority
Zep-Re Place, 7th Floor
Upper Hill, Longonot Road, off Kilimanjaro Avenue

P.O. Box 43505 GPO 00100, Nairobi Kenya
Tel: +254-20-4996000
Mobile: +254 - 719 047000
Email:commins@ira.go.ke

Help Desk
Toll-free Line: +254 - 0800724499
Email: customercare@ira.go.ke
complaints@ira.go.ke
ethics@ira.go.ke

Insurance Fraud Investigation Unit
Hotline: +254 - 707598455, +254 - 786595455
Email: ifiu@ira.go.ke

Policyholders Compensation Fund
Tel: +254-20-4996238
Email: info@pcf.co.ke

Insurance Regulatory Authority
Bima Bora kwa Taifa
IRA

MAHITAJI NA MANUFAA YA BIMA

MAHITAJI NA MANUFAA YA BIMA

Maana ya Bima

Bima ni njia moja ya kujikinga na matukio mbali mbali yanayotukumba maishani kila uchao. Bima ni mbinu mnununuzi hutumia ili kuhamishia kampuni ya bima mzigo wa hasara za kifedha. Ili apate kusimamiwa na kufidiwa na kampuni ya bima, mnunuzi sharti agharamie malipo ya bima ijulikanayo kwa Kiingereza kama premium. Kisha, bima hulipa fidia kwa mnunuzi huyo anapohusika kwenya tukio bila kutarajia na kupata hasara za kifedha.

Jinsi Bima inavyofanya kazi

Bima hufanya kazi katika msingi kwamba hasara na misiba hutukia mara kwa mara kwetu, kwa mali yetu au kwa jamii zetu. Bima huongozwa na busara kwamba ni vyema kujitayarisha mapema kwa tukio linaloweza kutokea bila kutarajiwa kuliko kungojea kuchukua hatua baada ya hasara kutokea. Bima huongozwa na msingi kwamba ni wachache tu kati ya wanunuzi bima ambao hupata hasara. Kwa mfano, ni magari machache tu ambayo hupotea kila mwaka au ni nyumba chache tu huchomeka. Vilevile, ni watu wachache tu huwa wagonjwa au kuhusika kwenya ajali. Hata hivyo, hakuna anayejua ni nani atakayehusika kwenye hasara. Kwa hivyo, ni jambo la busara sana kwa wote walio katika hatari ya kufikwa na hasara kuamua kulipa ada (premium) ili kujitayarisha kwa tukio lolote.

> **Bima ya maisha hulipa familia fidia kufuatia kifo au ulemavu kwa mwenye bima ambaye pia huenda akawa tegemeo la jamii.**

Sababu ya kununua bima

Hakuna aliye na uhakika kuhusu kinachoweza kutokea maishani mwake wakati wowote. Waweza kuvamiwa na wezi nyumbani au katika biashara yako; moto waweza kuteketeza nyumba au viwanda; ajali zinazohusisha magari au pikipiki zinaweza kutokea kisha kusababisha majeraha, vifo au ulemavu. Mara nyingi visa kama hivi vinapotokea, wanaoathiriwa hujipata katika hali ya unyonge moyoni na umaskini kifedha. Hawawezi kukabiliana na athari zinazofuata. Kwa hivyo, hawa hulazimika kuita harambee au kukopa pesa kutoka kwa marafiki na jamaa zao. Huenda ikawa marafiki na jamaa hao pia wana mahitaji yao za kibinafsi. Mara nyingi, walioathirika hupaswa kuuza mali ya familia yenye thamani kubwa kama vile mashamba au mifugo kwa bei ya hasara.

Madhumuni ya bima ni kuhakikisha kwamba pesa zitalipwa na kampuni za bima ili kusaidia kukabiliana na hasara.

Je, manufaa ya bima ni yapi?

Kulipwa fidia kufuatia hasara

Bima husaidia pakubwa katika kulipa mali iliyopotea ama kuharibiwa. Kwa hivyo bima hulipa fidia na kumrejesha mhathirika katika hali alimokuwa kifedha kabla ya tukio. Hivyo basi, bima inachangia sana kwa kuthibiti maendeleo ya jamii.

Kulinda familia

Bima ya maisha hulipa familia fidia kufuatia kifo au ulemavu kwa mwenye bima ambaye pia huenda akawa tegemeo la jamii. Bima pia hulipa fidia ikiwa mwenye bima amefaulu kuishi hadi mwisho wa kipindi cha bima. Malipo haya hutegemea sana, kiwango au kiasi cha pesa mlioafikiana na kampuni ya bima mlipokamilisha mkataba huo. Hiki kiwango yajulikana kwa kiwango kama sum assured.

Utulivu na amani moyoni

Wale waliochukua bima kawaida huwa na utulivu na amani moyoni kwa ajili watakapopatikana na tukio lolote kama magonjwa au kuhusika katika ajali. Kampuni ya bima itagharamia athari zozote za kifedha zitakazotokea hadi kiwango walivyoafikiana. Hivyo, bima huwapa wateja ujasiri na kuondoa wasiwasi unaohusiana na misiba au hasara hizo za ghafla.

Kuweka akiba

Unaweza kuweka akiba kwa malipo kidogo kidogo kupitia bima ya maisha au malipo ya uzeeni (pension). Bima ya maisha ni mkataba wa kudumu ambao hulipia kiasi fulani cha pesa kipindi cha bima kitakapokamilika au mwenye bima kuaga dunia kabla ya kipindi kukamilika. Ni jukumu la mnunuzi bima kuchagua kipindi cha bima. Njia kama hii huchochea mazoea ya watu kuwekeza kupitia bima kisha kutumia mapato ya akiba hii kwa siku zijazo ili kushughulikia mahitaji mbalimbali ya kifedha.